**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BUKIRIRO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu**
**Mkuu wa shule 0782383550/0764629304**
**Makamu Mkuu wa Shule 06255328114/0776657767**
**potron 0624097398/0756902723**
**Shule ya Sekondari BUKIRIRO**
**S.L.P. 58, RULENGE -NGARA**
**Tarehe** ...................

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi..........................**
**S.L.P..................................**
**..........................................**
Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BUKIRIRO HALMASHAURI YA NGARA MKOA KAGERA MWAKA ...............**
Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kid  to cha Tano katika Shule hii mwaka 2026 na atasoma tahasusi ya..................Kati ya tahasusi zifuatazo **HKL, HGL,** zinazofundishwa hapa shuleni.

1. Shule ya Sekondari Bukiriro ipo umbali wa Kilometa 62 Kusini Magharibi mwa Mji wa NGARA. Usafiri wa basi kutoka mjini NGARA unapatikana katika kituo cha mabasi NGARA, Nauli ni Shilingi 10000.Kama unatokea Mwanza panda mabasi ya Zube au Nyehunge na shukia Mji mdogo RULENGE Nauli ya Gari toka RULENGE mpaka shuleni ni shilingi 3000. Shukia kituo cha BUKIRIRO

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 8/7/2026 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe .............. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ......................

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1. Sare za Shule**

**i.** Sare ya shule hii ni suluari za rangi ya DARK BLUE mbili ( KITAMBAA KIZITO CHA ORIGINAL) mchono wa linda 1 chini tumup upana wa inchi 18 na ndefu zifunike kisigino

**ii.** Shati mbili za rangi nyeupe zenye mikono mirefu na zilizowekewa Alama ya namba Tano ya kirumi mabegani. Alama hiyo inawekwa kwa KITAMBAA Cha rangi ya dark blue.

**iii.** Sare ya Michezo ni jezi ya rangi ya blue bahari ( tishet na kaptula yake) pamoja na track suit za rangi ya blue bahari yenye nembo ya shule inaweza kupatikana shuleni( Koti na suruali yake) TSH 24000

**iv.** Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

**v.** Soksi jozi mbili nyeupe(nyeusi)

**vii.** Sweta mbili rangi ya dark blue.

**viii.** Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni suluari mbili za rangi ya kitambaa cha kaki Liwe la staha na KITAMBAA kizito pamoja na tshet ya BLUE yenye nembo ya shule inayoweza kupatikana shuleni, Tshs 15000

**ix.** Tai Moja ya dark blue ya pundamilia (mistari mweupe) inaweza kupatikana shuleni TSH 5000.

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

**i.** Madaftari makubwa (counter books) kumi.

**ii.** **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka. Aina ya ream ni **DOUBLE A**

**iii.** Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

**iv.** Scientific Calculato

**v.** Godoro la futi mbili na nusu, Kwa wanaotoka mbali maduka ya Rulenge mjini Yanapatikana.

**vi.** Mashuka Jozi 2 rangi ya bluu bahari, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi nyeupe,Taulo la kuogea

**vii.** Nguo za ndani za kutosha;

**viii.** Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

**ix.** Ndoo 2 ndogo za ujazo wa lita 10, zenye mifuniko na beseni.

**X. Vifaa vya usafi**

| S/N | COMBINATION/TAHASUSI | KIFAA CHA USAFI |
|---|---|---|
| 1 | HKL | Kwanja, jembe, fagio la nje, na soft blue, mopper |
| 2 | HGL | Kwanja, jembe,fagio la nje na toilet brush, mopper. |

**Xi.** Bima ya Afya ya NHIF au CHIF.

## 2.3 Michango mbalimbali Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| **Jumla** | **80,000** | |

**Tafadhali lipa kupitia akaunti ya shule ifuatayo**

**JINA LA AKAUNTI: BUKIRIRO SECONDARY CAPITATION**

**AKAUNTI: 32101200064**

**BENKI: NMB**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

- **i.** Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine najamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
- **ii.** Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana naratiba ya shule;
- **iii.** Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

**iv.** Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
**v.** Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
**vi.** Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
**vii.** Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
**viii.** Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
**ix.** Kutunza mali za shule;
**x.** Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
**xi.** Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

O **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

O **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

O **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

**i.** Wizi;
**ii.** Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
**iii.** Kugoma na kuhamasisha mgomo;

**iv.** Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
**v.** Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

**vi.** kuwa na nywele fupi wakati wote uwapo shuleni
**vii.** Kufuga ndevu;
**viii.** Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya
**ix.** Uvutaji wa sigara;
**x.** Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
**xi.** Kusababisha mimba;
**xii.** Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
**xiii.** Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
**xiv.** Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
**xv.** Kudharau Bendera ya Taifa;
**xvi.** Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
**xvii.** Uharibifu wamali ya umma kwa makusudi

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**
   **i.** Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
   **ii.** Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
   **iii.** Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
   **iv.** Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**BUKIRIRO TUNAAMINI KUWA UTAPATA ELIMU BORA NA KUWA MTU SAHIHI KWA JAMII YA KITANZANIA.**

**BUKIRIRO BILA DARAJA LA TATU,NNE NA SIFURI INAWEZEKANA,KARIBU UTIMIZE WAJIBU WAKO NA KUKAMILISHA NDOTO YAKO**

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**.........................................**

**AKWILINI S. GWIMBI**

**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
BUKIRIRO SEC. SCHOOL
NGARA

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao).**

**Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO WASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KWA NAMBA ZILIZOTAJWA HAPO JUU**

**SHULE YA SEKONDARI BUKIRIRO**
**FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE**

***(Ijazwe kwa herufi kubwa na kurejeshwa kwa mkuu wa shule)***

i. Jina kamili (mwanafunzi) ………………………………………………………………… Tarehe ya kuzaliwa ……………………….. Wilaya ……………….. Mkoa…… …......... Taifa ................................................Dini RC/Anglican/Lutheran/Muslim/Pentecosten.k Shule ya msingi unayotoka ..........................................................................................ii. Jina kamili la Baba/Mama/Mlezi ……………........................................Anwani yake…………………………. Kazi ya baba/Mama/Mlezi..........................................................................................Anwani yake……………………….………Namba ya simu……………………………….

**AHADI YA MWANAFUNZI.**

i. Mimi.......................................................................................... nimeyasoma na Kuyaelewa maelezo yote ambayo ni pamoja na sheria na kanuni za shule ni nimekubali kuingia kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Bukiriro kuanzia Tarehe ............... hadi nitakapomaliza kidato cha nne .

ii. Kwa hiyo naahidi kwamba:-
(a) Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.
(b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa shule na serikali ja Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kama kushiriki migomo ,Fujo,makosa ya jinai n.k.
(c) Nitatunza mali za UMMA ambazo ni pamoja na majengo na samani,vitabu n.k
Tarehe …………………………. Sahihi ya mwanafunzi……………………

**AHADI YA MZAZI/MLENZI**

Mimi …………………….. ambaye ni mzazi/mlenzi wa mwanafunzi ……………………….. nina ahidi kwamba :-
i. Nitashirikiana na uongozi wa shule , walimu na watumishi wasowalimu katika kuhakikisha mwanangu anatii sheria na kanuni za shule ya sekondari Bukiriro iwapo atashindwa kutii sheria hizo nitalazimika kukubaliana na adhabu itakayotolewa na uongonzi wa shule. ii. Nitafanya kila niwezalo kuwezesha mwanangu kusoma kwa bidii kama ilivyoelekezwe na shule.
Sahihi……………………………………………Tarehe ..............................................Namba ya simu……………………………………..……………………………….

**NGARA DISTRICT COUNCIL**
**BUKIRIRO SECONDARY SCHOOL**

## MEDICAL EXAMINATION

To be completed by Medical officer in respect of Bukiriro Secondary School student.(entarant)
1 Student's full name……………………………………

2 Sex…………………………………………………
3 HGB Test………………………………………

4 STOOL Test: ……………………………………..

5 URINE……………………………………………….

6 T.B Test: ……………………………………………..

7 EYE Examination: …………………… ……………….

8 E.N.T ……………………………………………………

9 CHEST……………………………… ……………….

10ABDOMEN ……………………………………………..

ADDITIONAL INFORMATION
Physical defects or impairments, infection, chronic or hereditary (family disease).
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
………………………………
I certify that I have examined the above student and discover that HE is physically NOT/fit for further studies.
NAME: ……………………………………………………………
SIGNATURE……………..……………………………………
DATE: ……………………………………………………

**OFFICIAL STAMP**